

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

JE INAFAA KUJITIBU KWA KUTUMIA MAFUTA YA NYOKA AU YA CHUI ?

01

فيه رجل يستعمل الحيات للطب، ويزعم أن ذلك مباح للظروف والضرورة، وطريقة استعماله في الحياة: يمسكها ويضعها في قدر سمن وهي لم تمت، والقدر يغلي على النار، وبعد ذلك يعالج بالسمن الذي طبخ فيه الحياة، والذي يستعمله يسكر سكرًا خفيفاً، هل يجوز التداوي بهذا السمن إذا ثبت أنه مفيد للمرض، وهل يجوز وضع الحياة بالسمن وهو يغلي على النار.

ج 1: أولاً: لا يجوز وضع الحيوان وهو حي في سائل يغلي؛ لما في ذلك من تعذيب الحيوان، وهو منهي عنه بقول النبي ﷺ: «إذا قتلتم فأحسنوا القتلة» (1) «الحديث. ثانياً: لا يجوز التداوي بالحيات ولا بالسمن الذي طبخت فيه؛ لأنها لا يجوز أكلها على الصحيح من قول العلماء، وميتتها نجمة، والتداوي بالمرح حرام.

SWALI

Kuna mtu ambaye anatumia nyoka katika kutibu, na anadai kwamba jambo hilo linafaa kwa dharura. Njia ya matumizi yake kwa nyoka huyo ni hii ifuatayo; anamkamata nyoka akiwa hai na anamuweka ndani ya chungu ambacho kipo jikoni kinachemka. Baada ya hapo anatibu kwa kutumia mafuta yaliyopatikana kwa uchemshwaji wa nyoka huyo, na mtumiaji wa dawa hiyo huwa analewa kiasi fulani. Je inafaa kujitibu kwa kutumia mafuta hayo endapo itathibitika kuwa ni dawa yenye kuponyesha maradhi; na je inafaa kuweka nyoka katika chungu kinachochemka motoni?

JAWABU :

‘Kwanza kabisa: Haifai kuweka mnyama yeyote aliye hai ndani ya maji yachemkayo, kwa sababu katika hilo kuna kumuadhibu mnyama (kwa moto), na hilo ni jambo ambalo limekatazwa kwa kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam aliposema: ((Na pindi mnapoua basi fanyeni wema katika mauaji)).

02

Pili: Haifai kujitibu kwa kutumia nyoka wala kwa kutumia mafuta ambayo yametokana na nyoka aliyechemshwa, kwa sababu haifai kumla nyoka kwa mujibu wa kauli sahihi miongoni mwa kauli mbili za wanachuoni , na mzoga wa nyoka ni najisi , na kujitibu kwa kitu haramu , ni haramu (haifai).’

يوجد في الأسواق ما يسمى (شحم النمر) فهل يجوز استخدامه للعلاج ونحوه؟

ج 2: لا يجوز تعاطي شحم ما حرم الله أكله ولو كان للعلاج، ومن ذلك النمر؛ لأن له ثابتاً يفترس به، وقد «حرم النبي ﷺ كل ذي ناب من السباع.

SWALI

Masokoni yanapatikana mafuta yaitwayo mafuta ya chui. Je inafaa kuyatumia mafuta hayo na mfano wake kwa kujitibu ?

JAWABU:

‘ Haifai kujitibu kwa kutumia mafuta ya kile ambacho Allah ameharamisha uliwaji wake, na miongoni mwake ni chui. Kwa sababu chui ana meno ya kuwindia; na ameharamisha Mtume swallallaahu alaihi wasallam kula mnyama yeyote mwindaji mwenye meno ya kuwindia.’

Mwisho

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

المراجع: فتاوى اللجنة الدائمة